**Shindano la Nne la Stadi za Ufundishaji kwa Walimu wanaofundisha Shule za Awali na Msingi, na la Pili kwa walimu wanaofundisha Shule za Sekondari Tanzania Bara**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inawaalika na kuwahamasisha walimu wanaofundisha Darasa la Awali, na Darasa la kwanza kwa Shule za Msingi, na Kidato cha kwanza kwa shule za Sekondari za Serikali zilizopo katika halmashauri zote Tanzania Bara kushiriki katika shindano la stadi za ufundishaji la nne kwa walimu wanaofundisha Darasa la awali na msingi na la pili kwa walimu wa wanaofundisha kidato cha kwanza kwa shule za sekondari katika masomo ya *Physics, Mathematics, Computer Science*, na Business studies, na umahiri wa Kumudu stadi za awali za kusoma na *Demonstrate mastery of basic English language skills.*

**Maeneo ya kushindania**

**Elimu ya Awali:**
**Umahiri: Kumudu stadi za awali za kusoma**

- Kufundisha sauti za herufi (g, y, z, h, r, w, v, ch)

**Elimu ya Msingi:**
**Umahiri: Demonstrate mastery of basic English language skills**

- Pronounce one of the following English sounds:
  Consonants: /θ/ for "th", /ð/ for "th", /ʃ/ for "sh", /tʃ/ for "ch", /l/ for l, /r/ for r, /z/ for z, /v/ for v, /f/ for f, /s/ for s
  Vowels: /ʌ/ for "u", long vowels, such as /iː/, /uː/, /ɔː/

**Elimu ya Sekondari:**
**Somo: Physics**

- Describe the concept of motion under gravity

**Somo: Mathematics**

- Recognising the point of intersection of two linear equations

**Somo: Computer Science**

- Create an algorithm for a familiar real-life problem by analysing it, arranging the solution into logical steps, and representing it in both pseudocode and a correctly drawn flowchart.

**Somo: Business Studies**

- Explain how to establish a startup, specifically a sole proprietorship

**Jinsi ya kushiriki**

- Mwalimu anapaswa kuandaa andalio la somo la dakika 10 hadi 15 linalozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi kuendana na mtaala ulioboreshwa wa mwaka 2023 na kuliweka kwenye mfumo wa pdf.
- Kutumia andalio hilo kufundishia wanafunzi Darasani.
- Kurekodi video ya kipindi anachofundisha.
- Kipindi kitakachofundishwa kizingatie matumizi ya mbinu shirikishi zinazolenga kukuza stadi za karne ya 21.
- Video za kipindi kilichorekodiwa zitawasilishwa Taasisi ya Elimu Tanzania kupitia link: https://tie-teachers-competition.vercel.app/
- Video zitaanza kupokelewa kuanzia tarehe 9/12/2025 hadi 30/1/2026

**Zawadi kwa washindi**

1. Mshindi wa kwanza atapata Tsh 2,500,000/=, Kitendea kazi na cheti cha pongezi. Shule itapata kitendea kazi (projector)
2. Mshindi wa pili atapata Tsh 2,000,000/=, Kitendea kazi na cheti cha pongezi. Shule itapata kitendea kazi (projector)
3. Mshindi wa tatu atapata Tsh 1,500,000/=, Kitendea kazi na cheti cha pongezi. Shule itapata kitendea kazi (projector)
4. Mshindi wa nne na tano watapata cheti cha ushiriki.

Aidha, Washindi wote maudhui yao ya video yatarekodiwa tena katika studio za TET na kupakiwa katika mfumo wa elimu wa kidigitali (Learning Management System-LMS) na kurushwa kwenye TET Soma Kwanza TV.

Kwa mawasiliano piga simu namba: 0717489559, 0754271767, au 0763788809

**Vigezo vya shindano la stadi za ufundishaji kwa shindano la pili (Sekondari) na nne (Madarasa ya awali na msingi)- 2025/2026**

Vigezo vifuatavyo vitazingatiwa wakati wa kufanya tathmini ya video za shindano la stadi za ufundishaji:

**A. Mshiriki**

1. Awe mtanzania
2. Awe mwalimu anayefundisha shule ya serikali katika ngazi ya shule za awali, msingi au sekondari.
3. Awe mwalimu mwenye ajira ya kudumu na awe na check namba
4. Awe mwalimu ambaye hajawahi kushiriki shindano lolote lililopita na kuwa mshindi.

**B. Video/kipindi**

1. Video ya kipindi isiyopungua dakika 10 na kuzidi dakika 15.
2. Uwepo wa andalio la somo linalozingatia muhtasari wa ngazi husika ya darasa, kanuni za uandaaji wa andalio kama vile IDDR model na uchopekaji wa 5Es.
3. Matumizi ya mbinu shirikikishi na zana za ujifunzaji (Namna wanafunzi wanavyoshirikishwa katika ujifunzaji kwa vitendo huku wakitumia zana za ujifunzaji).
5. Uchopekaji wa TEHAMA na masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji.
6. Matumizi ya mbinu za upimaji na utoaji mrejesho katika kuimarisha ujifunzaji
7. Uwezo wa kumudu darasa na kulifanya kuwa salama, changamshi na jumuishi katika kufikia lengo la ujifunzaji.

8. Matumizi ya lugha sahihi na inayoeleweka pamoja na matumizi ya lugha ya mwili na sauti inayosikika.
9. Uwezo wa kuunganisha nadharia na vitendo, uelewa wa kina wa somo na uweledi na maadili ya ufundishaji.